**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**
**VETA IRINGA**

---

**BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO NGAZI YA KWANZA**

**IRINGA RVTSC**

**2024**

Ndugu,

............................................................................................................................

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA IRINGA (RVTSC) MWAKA 2024**

**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MKLEZI NA MWANAFUNZI**

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika
2. Fani ya: ..............................................................................................................
   Ngazi ya Kwanza (Level One) Kutwa/Bweni

3. Mafunzo yatachukua muda wa miaka mitatu kwa ngazi ya tatu kwa fani ya Upishi na Huduma ya chakula na vinywaji, miaka miwili na nusu kwa ngazi ya tatu kwa fani ya Uhazili na miaka miwili kwa ngazi ya pili kwa fani nyingine.

4. Chuo kitafunguliwa Rasmi Tarehe **15/01/2024**
5. Unatakiwa kudhibitishwa na daktari wa hospitali ya serikali kuwa una afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa kwa kujaza fomu maalum (medical examination form) iliyoambatanishwa.

6. Unatakiwa kudhibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye barua hii.
7. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii mara utakapofika chuoni.
8. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
9. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
10. Unatakiwa kuleta kivuli cha cheti cha kumaliza shule
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo.

## MAHITAJI YA MWANAFUNZI ATAKAPORIPOTI CHUONI

*Unatakiwa uwe na vifaa vifuatavyo:*

1. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi ya "Tetron" ***Kwa wavulana tu***
2. Jozi moja ya viatu vyeusi vya Ngozi vyenye visigino vifupi
3. Daftari 8 kubwa
4. Vifaa vya somo la Hesabu (Mathematical set)
5. Karatasi nyeupe (A4) ream moja
6. Sweta rangi ya Blue
7. Soksi rangi nyeupe au nyeusi
8. Viatu vya karakana aina ya "Safety boots" kwa ajili ya usalama utakapokuwa karakana
9. Kwa mwanafunzi wa bweni awe na godoro la futi (3 kwa 6) mto wa kulalia, blanketi, shuka 2 za rangi ya blue na foronya zake, chandarua, ndoo, sahani, kikombe, kijiko, nguo za kujikinga na baridi utakapokuwa bwenini, pamoja na vifaa vya usafi binafsi.

**MCHANGANUO WA MALIPO**

| NA | MAHITAJI | | KWA MWANAFUNZI WA KUTWA | | KWA MWANAFUNZI WA BWENI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | MUHULA I | MUHULA II | MUHULA I | MUHULA II |
| 1. | Ada | | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 |
| 2. | Bima ya afya | | 50,400 | | 50,400 | |
| 3. | Suruali (2) za chuo | | 40,000 | | 40,000 | |
| 4. | Overcoat/Overall/Chef jacket | | 30,000 | | 30,000 | |
| 5. | Fulana/T-shirt | | 15,000 | | 15,000 | |
| 6. | Kitambulisho | | 5,000 | | 5,000 | |
| 7. | Nembo za VETA | | 5,000 | | 5,000 | |
| 8. | Michezo | | 15,000 | | 15,000 | |
| 9. | Uchakavu na Mazingira | | 20,000 | | 20,000 | |
| 10 | Picha (passport size) | | 3,000 | | 3,000 | |
| 11 | Blouse (2) -***kwa wasichana tu*** | | 30,000 | | 30,000 | |
| | JUMLA | Wavulana | **213,400** | | **243,400** | |
| | | Wasichana | **243,400** | | **273,400** | |

ZINGATIA:

I. Malipo yote yatafanyika chuoni kupitia namba ya malipo ya serikali "control number" utakayopewa mara utakaporipoti chuoni. Baada ya kulipa fedha benki mwanachuo aje na risiti ya benki ikabidhiwe ofisi ya msajili.

II. Kama unayo bima ya afya uliyopewa kupitia mzazi/mlezi hupaswi kulipa fedha ya bima, unatakiwa uje na kitambulisho chako kwa ajili ya uhakiki.

III. Kutakuwa na Malipo kwa ajili ya mtihani wa ngazi ya kwanza sh.25,000 yatakayolipwa katikati ya muhula wa pili kupitia namba maalumu ya malipo "control number" utakayopewa wakati huo.

***IV.*** Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa kwenye barua hii. Hutapokelelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa fedha kiasi ulichoagizwa tu. ***Fedha ikishalipwa hairudishwi***

MAELEZO MENGINE UTAELEKEZWA UFIKAPO CHUONI

.........................................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
NA HUDUMA
S.L.P 778 IRINGA

PASIENS NAZARY NYONI

MKUU WA CHUO

VETA IRINGA

**VIAMBATANISHO**

I. Medical Examinations form

II. Sheria za chuo

III. Fomu ya kukubali nafasi ya mafunzo ya ufundi

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi ........................................................................................................................ ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Namba za simu ya mwanachuo 1: ................................ 2: ....................................

Saini ya mwanachuo .................................. Tarehe..........................................

b) MDHAMINI

Mimi..........................................................................................................................
ni.................................................................................ambaye
.................................................. wa mtajwa hapo juu, nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Namba za simu ya mdhamini 1:................................ 2:..................................

Saini ya mdhamini ........................................... Tarehe..........................................

*VET MED FORM – 1E*

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date ..........................................................

The Medical Officer

..........................................................

..........................................................

..........................................................

### REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

Name of trainee ..........................................................

Please Examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an ..........................................................

Eyesight ..........................................................

Hearing ..........................................................

Asthma ..........................................................

Other serious diseases ..........................................................

### MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date.......................................................... Designation ..........................................

Signature and Official stamp ..........................................................